**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

Ofisi ya Bunge
S.L.P 941
**DODOMA**

11 APRILI, 2018

## YALIYOMO

**1.0 UTANGULIZI ........................................................ 1**

**2.0 MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA NA KUTEKELEZWA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 ........................................................ 5**

2.1 Ufafanuzi wa Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 .................... 5

2.1.1 Mradi Na. 6405 Programu ya Uimarishaji Miji (ULGSP) ........................................ 5

2.1.2 Mradi Na. 4946 - Local Government Own Source Projects "Uwezeshaji Kiuchumi Wanawake na Vijana". ........................................ 6

2.1.3 Mradi Na. 4946 – Local Government Own Source Project (Mfumo wa Ukusanyaji Mapato kwa njia ya Kieletroniki - *LGRCIS*) ........................................ 7

2.2 Matokeo ya Ukaguzi ........................................ 8

2.2.1 Mradi Na. 6405 Program ya Uimarishaji Miji (ULGSP) ........................................ 8

2.2.2 Mradi Na. 4946 - Local Government Own Source Projects.(Uwezeshaji Kiuchumi Wanawake na Vijana) ........................................ 9

2.2.3 Mradi Na. 4946 - Local Government Own Source Projects (Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani kwa njia ya Kielektroniki). ........................................ 10

2.3 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018... 12

**3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 ........................................ 14**

3.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.... 14

3.1.1 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu ukusanyaji Maduhuli ........................................ 14

3.1.2 Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina ........................................ 16

3.1.3 Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati ........................................ 19

**4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 ........................................ 23**

4.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 ........................................ 23

4.2 Uchambuzi wa makadirio ya Mapato ........................................ 26

4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi ........................................ 28

**5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI ........................................ 31**

**6.0 HITIMISHO ........................................ 36**

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

---

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 6(4) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 Kamati hii ina jukumu la kuisimamia Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (OR - UUB) pamoja na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI). Aidha, Kifungu cha 7(1) (a), kinafafanua jukumu mahususi la Kamati kushughulikia Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

**Mheshimiwa Spika**, kabla ya kuanza uchambuzi wa bajeti, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, ambayo yanaielekeza Kamati kwa siku zisizozidi saba (7) kufanya ziara ya ukaguzi wa Miradi ya maendeleo iliyotekelezwa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa Mwaka wa Fedha unaoisha.

Kamati ilitekeleza jukumu hilo na kisha kuingia katika uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi hii kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Taarifa hii inahusisha mapitio na uchambuzi wa jumla ya Mafungu Ishirini na Nane (28) yafuatayo:-

i. Fungu 56: Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;
ii. Fungu 02: Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC);
iii. Fungu 70 – Mkoa wa Arusha;
iv. Fungu 88 – Mkoa wa Dar es Salaam;
v. Fungu 63 – Mkoa wa Geita;
vi. Fungu 78 – Mkoa wa Mbeya;
vii. Fungu 90 – Mkoa wa Songwe;
viii. Fungu 89 – Mkoa wa Rukwa;
ix. Fungu 80 – Mkoa wa Mtwara;
x. Fungu 85 – Mkoa wa Tabora;
xi. Fungu 84 – Mkoa wa Singida;
xii. Fungu 75 – Mkoa wa Kilimanjaro;
xiii. Fungu 71 – Mkoa wa Pwani;
xiv. Fungu 36 – Mkoa wa Katavi;
xv. Fungu 81 – Mkoa wa Mwanza;
xvi. Fungu 73 – Mkoa wa Iringa;
xvii. Fungu 87 – Mkoa wa Kagera;
xviii. Fungu 54 – Mkoa wa Njombe;
xix. Fungu 74 – Mkoa wa Kigoma;
xx. Fungu 76 – Mkoa wa Lindi;
xxi. Fungu 95 – Mkoa wa Manyara;
xxii. Fungu 77 – Mkoa wa Mara;

xxiii. Fungu 47 – Mkoa wa Simiyu;
xxiv. Fungu 86 – Mkoa wa Tanga;
xxv. Fungu 72 – Mkoa wa Dodoma;
xxvi. Fungu 82 – Mkoa wa Ruvuma;
xxvii. Fungu 83 – Mkoa wa Shinyanga; na
xxviii. Fungu 79 **-** Mkoa wa Morogoro;

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa Taarifa mbele ya Bunge lako Tukufu kuwa baada ya Kamati hii kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa Fedha unaoisha pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti kwa mwaka wa Fedha unaoanza, Taarifa hii ya Kamati kuhusu Ofisi ya Rais – TAMISEMI inajikita katika maeneo manne (4) yafuatayo:-

i) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotembelewa na Kamati;

ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;

iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019; na

iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, Rais wa zamani wa Afrika Kusini, Thabo Mvuyelwa Mbeki wakati akielezea sera za taifa hilo na maendeleo yanayoweza kuletwa na Serikali za Mitaa, aliwahi kusema maneno yafuatayo, na hapa ninanukuu;

> *"…the policies might be there but are people benefiting from the policies? You find that in many instances, though the policies exist, they are not having the necessary impact. That is a particular challenge in Local Governmet, because that is where all the services get deliverd."*

Kwa tafsiri isiyo rasmi anachokisema Thabo Mbeki ni kwamba;

> *"Sera zinaweza kuwepo, lakini watu wananufaika nazo? Katika matukio mengi utakuta kwamba, ingawa sera zipo lakini hazina tija. Hiyo ndiyo changamoto haswa katika Serikali za Mitaa, kwa sababu ndiko huduma zinakotolewa."*

**Mheshimiwa Spika,** lengo la kunukuu maneno hayo ni kutokana na ukweli kwamba, nchi yetu pia ni miongoni mwa Mataifa ambayo yaliamua kutekeleza Sera ya Ugatuaji wa Madaraka *(Decentralization by Devolution)* kutoka Serikali kuu kwenda Serikali za Mitaa. Lengo la ugatuaji huo ni kusogeza huduma kwa wananchi katika ngazi za chini. Hata hivyo, lengo hilo linaposhindwa kutekelezwa ndipo wananchi wanapohoji maana nzima ya kutekeleza dhana ya ugatuaji wa madaraka.

Kwa mantiki hiyo, Serikali inapaswa kuandaa mikakati na mipango thabiti ya uboreshaji wa huduma muhimu za kijamii katika ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, ili kufanikisha azma ya kuboresha maisha ya Watanzania na kuwa na maendeleo endelevu kwa Taifa letu.

## 2.0 MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA NA KUTEKELEZWA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

### 2.1 Ufafanuzi wa Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, iliidhinishiwa na Bunge jumla ya **Shilingi 1,783,206,586,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

Ili kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitembelea na kukagua baadhi ya Miradi ya Maendeleo iliyotekelezwa na Ofisi hii katika Mwaka wa Fedha 2017/2018. Miradi hiyo ni pamoja na, Programu ya Uimarishaji Miji *(Urban Local Government Authorities Strengthening Program - ULGSP)* ; Mfuko wa Maendeleo wa Vijana na Wanawake (Asilimia 10 ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri) pamoja na Mfumo wa Ukusanyaji Mapato ya Ndani kwa njia ya Kieletroniki *(Local Government Revenue Collection Information System - LGRCIS)* kama ifuatavyo:-

#### 2.1.1 Mradi Na. 6405 Programu ya Uimarishaji Miji (ULGSP)

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu ulitengewa jumla ya **Shilingi 3,328,956,000** na ulipangwa kutekelezwa chini ya Kifungu 8091 cha **Fungu 83** – Mkoa wa Shinyanga.

Mradi huu ambao unalenga kuendeleza miundombinu ya barabara katika Halmashauri ya Shinyanga, unahusisha ujenzi wa barabara yenye urefu wa Kilomita 13.1 kwa kiwango cha lami. Hadi wakati

Kamati inatembelea mradi huu kilomita 4.37 zilikuwa zimekamilika, hii ikiwa ni sawa na asilimia 33.4 ya utekelezaji wa mradi.

Aidha, mradi utahusisha **ujenzi wa** mifereji rafiki kwa ajili ya maji taka, ujenzi wa njia za waenda kwa miguu, uwekezaji wa taa na alama za barabarani.

2.1.2 **Mradi Na. 4946 - Local Government Own Source Projects "Uwezeshaji Kiuchumi Wanawake na Vijana**".

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu ulitengewa jumla ya **Shilingi 471,452,580/=** na ulipangwa kutekelezwa chini ya Kifungu 8091 cha **Fungu 47** - Mkoa wa Simiyu. Mradi huu ni sehemu ya jitihada za Serikali za kuwawezesha Kiuchumi Wanawake na Vijana, kupitia asilimia (10%) ya mapato ya ndani ya kila Halmashauri nchini. Kupitia utaratibu huu Wanawake na Vijana wamejengewa uwezo wa kubuni miradi na kupata mitaji ya kuitekeleza na hivyo kujikwamua kiuchumi.

Kamati ilitaka kujiridhisha na utekelezaji wa Mradi huu na hivyo ilitembelea Kikundi cha Vijana ambacho kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Maswa kimeanzisha Kiwanda cha Chaki kilichopo Maswa Mjini. Katika Kiwanda hicho, Kamati ilipata fursa ya kujionea shughuli za uzalishaji na ufungashaji *(production and packaging)*.

Aidha, Kamati ilielezwa kwamba katika mradi huo wa ubia ambao una mtaji wa thamani ya **Shilingi Milioni 100**, Kikundi hicho cha vijana kinamiliki asilimia 40 ya hisa na Halmashauri ya Wilaya ya Maswa inamiliki asilimia 60.

Vijana hao walianza na mtaji wa **Shilingi 1,000,000** kabla ya kupata fedha kutoka mfuko wa uwezeshaji wa Vijana wenye thamani ya **Shilingi Milioni 30**.

Aidha, mradi huo umeingizwa katika kundi la miradi ya kimkakati ya Halmashauri na umetengewa kiasi cha **Shilingi Bilioni 4** kwa ajili ya upanuzi wa Kiwanda hicho na kuanzisha uzalishaji wa bidhaa nyingine za kimkakati kama vile vifaa tiba na vifaa vya ujenzi.

### 2.1.3 Mradi Na. 4946 – Local Government Own Source Project (Mfumo wa Ukusanyaji Mapato kwa njia ya Kieletroniki - *LGRCIS*)

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu ulipangwa kutekelezwa chini ya Kifungu 8091 cha **Fungu 85** - Mkoa wa Tabora. Lengo la mradi huu ni kuiwezesha Serikali kuongeza mapato kwa kuboresha njia na Mfumo wa ukusanyaji wa mapato *(revenue collection system)*.

Kupitia mradi huu Serikali imeachana na matumizi ya vitabu na Mawakala katika ukusanyaji wa mapato, jambo ambalo limewezesha kuepuka upotevu mkubwa wa mapato kutokana na upotevu wa kumbukumbu na mawakala wasio waaminifu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa uamuzi na kasi ya kuanzisha Mfumo huu ambao sasa unatumika katika Halmashauri zote 185 nchini. Mfumo wa ukusanyaji mapato ya ndani kwa njia ya kielektroniki *"Local Government Revenue Collection Information System"* ulianzishwa rasmi katika mwaka wa fedha 2016/2017.

Kamati ilielezwa kuwa katika mwaka wa fedha (2017/2018) Halmashauri ya Manispaa ya Tabora ilipanga kukamilisha lengo la ununuzi wa mashine 85 za kukusanyia mapato (POS). Hadi wakati Kamati inakagua utekelezaji wa Mfumo huo tayari Halmashauri ilikuwa imeishanunua mashine 59, sawa na asilimia 69.4 ya lengo.

**Mheshimiwa Spika,** ili kujiridhisha na matumizi ya mfumo huu Kamati iliweza kutembelea na kukagua maeneo ya biashara katika

Soko kuu la Tabora lenye jumla ya mashine 9 za kukusanyia mapato *(POS),* na Stendi ya Mabasi yaendayo Mikoani ambayo inatumia mashine mbili tu za POS.

## 2.2 Matokeo ya Ukaguzi

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo hiyo inayotekelezwa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, naomba kutoa Taarifa kwa Bunge lako Tukufu juu ya mambo ambayo Kamati iliyabaini kama ifuatavyo:-

### 2.2.1 Mradi Na. 6405 Program ya Uimarishaji Miji (ULGSP)

**Mheshimiwa Spika,** katika Halmashauri ya Shinyanga ambako Kamati iliweza kutembelea na kukagua utekelezaji wa mradi huu wa kuimarisha miundombinu, ukaguzi huo ulibaini mambo yafuatayo:-

a) **Mafanikio;**

i) Kuongezeka kwa mtandao wa barabara za lami katikati ya Mji wa Shinyanga;

ii) Kuongezeka kwa biashara na uwekezaji katika maeneo ya kati ya Mji kutokana na kuboreshwa kwa miundombinu ya barabara; na

iii) Kuongezeka thamani kwa maeneo ya makazi yaliyo jirani na barabara zinazojengwa.

b) **Changamoto;**

i) Kasoro za Mkataba kati ya Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga na Mkandarasi, zinachelewesha mradi huo na hivyo kuongeza gharama za utekelezaji;

ii) Usanifu wa awali *(feasibility study)* wa mradi haukuzingatia mahitaji halisi ya wakazi wa maeneo mradi unapotekelezwa;

iii) Mradi kutekelezwa kwa gharama kubwa ikilinganishwa na ubora wa kazi;

iv) Mifereji (mifereji rafiki) ya maji ambayo itakuwa inajaa udongo kwa urahisi na hivyo kushindwa kusafirisha maji taka kutokana na kujengwa chini ya kiwango;

v) Halmashauri kukosa wahandisi wa ujenzi na hivyo kukosa usimamizi madhubuti wa miradi ya barabara;

vi) Ushirikiano hafifu baina ya Halmashauri na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (*TARURA)*; na

vii) Uwepo wa viashiria vya rushwa katika utoaji wa zabuni za ujenzi wa mradi huo.

2.2.2 **Mradi Na. 4946 - Local Government Own Source Projects.(Uwezeshaji Kiuchumi Wanawake na Vijana**)

**Mheshimiwa Spika,** katika ukaguzi uliofanywa na Kamati katika mradi huu uliopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Maswa, mambo kadhaa yalibainika ikiwa ni pamoja na mafanikio na changamoto.

**(a) Mafanikio;**

i. Ajira za moja kwa moja na fursa ya kumiliki hisa kwa Vijana ambapo Vijana 28 wameajiriwa na kati

ya hao 6 wanamiliki hisa katika kiwanda hicho;

ii. Mradi huu ni miongoni mwa vyanzo vya mapato vya Halmashauri;

iii. Kiwanda hiki kimeweza kusambaza chaki katika Mikoa Nane (8) ya Tanzania Bara na Zanzibar na hivyo kupunguza matumizi ya chaki kutoka nje;

iv. Mradi huo umekuwa chachu ya Halmashauri nyingi kuanzisha Viwanda vya aina hii kutokana na kuwa sehemu ya mafunzo.

(b) **Changamoto;**

i. Teknolojia duni ambayo inafanya Kiwanda hicho kuzalisha chini ya kiwango;

ii. Kukosekana kwa malighafi mkoani Simiyu, na hivyo kulazimika kuzifuata mkoani Singida; na

iii. Mazingira ya ushindani yasiyo sawa yanayosababishwa na uingizaji wa chaki kutoka nje ya nchi.

2.2.3 **Mradi Na. 4946 - Local Government Own Source Projects (Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani kwa njia ya Kielektroniki**).

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu unatekelezwa katika Halmshauri zote nchini, lakini Kamati iliweza kutembelea Halmashauri ya Manispaa ya Tabora na kubaini mafanikio na changamoto kama ifuatavyo:-

**(a) Mafanikio;**

i. Mfumo wa *LGRCIS* umerahisisha utunzaji wa kumbukumu na hivyo kupunguza upotevu wa taarifa muhimu za hesabu;

ii. Kupunguza gharama za ukusanyaji mapato;na

iii. Mfumo umeongeza uwazi na hivyo kuiwezesha Serikali kudhibiti ubadhirifu wa mapato uliokuwa unasababishwa na Mawakala wasio waaminifu.

**(b) Changamoto;**

i. Matatizo ya mtandao kukata wakati wa kutoa huduma kwa wateja, hivyo kuathiri ukusanyaji wa mapato ;

ii. Mfumo wa *LGRCIS* kushindwa kuzungumza na Mifumo ya Benki na hivyo kuzifanya Benki kushindwa kuingiza malipo kwenye Mfumo kwa njia ya CHEQUE na TISS;

iii. Kukosekana kwa Wakala wa Benki kwa ajili ya makusanyo ya mapato ya Halmashauri; na

iv. Mfumo kushindwa kudhibiti taarifa za Halmashauri moja kuingiliana na taarifa za Halmashauri nyingine.

## 2.3 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo katika Mikoa ya Shinyanga, Simiyu na Tabora, Kamati iliweza kubaini mambo mbalimbali na inapenda kuyatolea maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

i. Hazina itoe fedha za Miradi ya Maendeleo kwa wakati ili kutoathiri utekelezaji wa miradi iliyopangwa na hivyo kuendelea kuwakosesha wananchi huduma zilizokusudiwa;

ii. Wanasheria wa Halmashauri wajengewe uwezo katika eneo la Sheria za Mikataba *(law of contracts)* ili kuziwezesha Halmashauri kuingia mikataba yenye manufaa kwa Taifa na kuepukana na ubadhilifu;

iii. Ushirikishwaji mdogo wa Wananchi katika uibuaji na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo *(feasibility study)* umeendelea kuathiri utekelezaji wa miradi hiyo, kutokana na Wananchi kujiona kwamba siyo sehemu ya miradi hiyo;

iv. Kukosekana kwa programu endelevu ya elimu ya ujasiriamali na uwezeshaji kwa Vijana kumefanya idadi kubwa ya vikundi hivyo vishindwe kutumia vizuri fedha za mikopo;

v. Urasimu *(cumbersome procedures)* usio wa lazima Serikalini umeendelea kuchelewesha utekelezaji wa miradi. Mfano, utaratibu wa watoa huduma na wakandarasi kuwasilisha madai kwa njia ya cheti *(certificates)* umekuwa

ukichelewesha malipo na hivyo kukwamisha utekelezaji wa miradi;

vi. Kukosa umakini katika usanifu wa awali *(feasibility study)* wa Miradi ya Maendeleo kunaathiri utekelezaji na hivyo kuongeza gharama; na

vii. Mfumo wa ukusanyaji na usimamizi wa mapato kwa nja ya Kieletroniki *(LGRCIS)* umeonesha mafanikio makubwa kwa kuongeza na kudhibiti mapato ya Halmashauri nchini. Hata hivyo, mfumo huu unahitaji maboresho ili kuondoa dosari zilizobainika.

## 3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

### 3.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati katika utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ulizingatia makusanyo ya maduhuli kwa kulinganisha na malengo na mwenendo wa upatikanaji wa fedha za matumizi kwa ajili ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa.

Njia zilizotumika katika uchambuzi huu ni kwa kuangalia hali halisi, kuzingatia taarifa mbalimbali zilizowahi kuwasilishwa kwenye Kamati, pamoja na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu wakati vikao vya Kamati.

Kwa ufafanuzi wa ziada kuhusu uchambuzi huu, Kamati imetumia majedwali ili kurahisisha maelezo yake wakati wa kuonesha taarifa, asilimia, ulinganishaji na utofautishaji.

#### 3.1.1 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu ukusanyaji Maduhuli

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2017/18 Ofisi ya Rais – TAMISEMI (Fungu 56) pamoja na Taasisi zilizo chini yake ilipanga kukusanya jumla ya Shilingi **22,766,063,908** kutoka vyanzo vya ndani. Kwa Fungu 56 mapato yalikadiriwa kukusanywa kutoka kwenye mauzo ya vifaa chakavu na zabuni. Aidha, kwa upande wa Taasisi mapato yalitarajiwa kutokana na tozo mbalimbali, ukusanyaji wa madeni, nauli za mabasi, ada za Wanafunzi katika Vyuo, ushuru wa

mauzo ya bidhaa mbalimbali, na kodi ya pango kwa wapangaji wa majengo ya Taasisi.

Hadi kufikia Februari, 2018 jumla ya **Shilingi 9,951,491,965.88** zilikuwa zimekusanywa na Fungu 56, kiasi ambacho ni sawa na **asilimia 43.7** ya mapato yaliyotarajiwa kukusanywa katika Mwaka wa Fedha 2017/18. Kamati ilitaka kujua ni kwanini kumekuwa na makusanyo hafifu ya maduhuli, na sababu zilizotolewa ni pamoja na:-

i. Mauzo machache ya nyaraka za zabuni na vifaa chakavu vya Ofisi;

ii. Halmashauri nyingi kushindwa kuwasilisha michango yao kwenye Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa;

iii. Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa kushindwa kupata **Shilingi Bilioni 1.2** ilizotarajia kuzipata kutoka CRDB;

iv. Kukosekana kwa ubunifu wa vyanzo vipya vya mapato.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi unaonesha kwamba, kiasi kilichokusanywa kimeongezeka kwa asilimia 15.7 ikilinganishwa na kiasi kilichokusanywa katika kipindi kama hicho kwa Mwaka Fedha 2016/2017 ambacho kilikuwa ni asilimia 28.13.

Ingawa kiwango kilichokusanywa kimeshindwa kufikia angalau asilimia 70 ambayo ilipaswa kuwa imefikiwa katika robo ya tatu, bado ni kikubwa hasa kwa kuzingatia kwamba malengo yaliyowekwa yalikuwa ni makubwa zaidi ikilinganishwa na malengo ya mwaka wa fedha uliotangulia.

Aidha, Kamati inatia shaka iwapo kwa kipindi kilichobaki malengo ya makusanyo yatafikiwa. Hii inatoa taswira kwamba bado Ofisi ya Rais, TAMISEMI haijaweza kuwa na makadirio sahihi kuhusu kiasi cha mapato kinachotakiwa kukusanywa au kuna uzembe wa ukusanyaji wa mapato. Tafsiri ya mtazamo huu ni kwamba, utekelezaji wa shughuli zilizopangwa na Ofisi hii kwa kutegemea fedha za ndani utaendelea kusuasua.

Kamati inaendelea kushauri kwamba, Ofisi ya Rais – TAMISEMI izingatie makadirio halisi ya makusanyo kutokana na vyanzo vilivyopo ili kuweza kuwa na makusanyo halisi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Mikoa na Serikali za Mitaa hadi kufikia mwezi Februari, 2018 makusanyo yalikuwa ni **shilingi 347,186,363,928,** kiasi ambacho ni sawa na asilimia 50 ya lengo.

Ingawa kiasi hiki kiko chini ya lengo la angalau asilimia 70 hadi kufikia robo ya tatu ya mwaka wa fedha, bado kiwango cha makusanyo katika Serikali za Mitaa kimeonekana kuwa kikubwa. Sababu inaweza kuwa ni kutokana na Halmashauri kuwa na vyanzo vingi vya makusanyo na wingi wa watu ikilinganishwa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI pamoja na Taasisi zake.

### 3.1.2 Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, umebaini kwamba, hakuna ulinganifu kati ya kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa Mwaka wa Fedha 2017/18 na kiasi kinachotolewa na Hazina.

Kutokana na uchambuzi huo Kamati imebaini kwamba:-

i. Fedha zinazotolewa ni kidogo ikilinganishwa na Mpango wa upatikanaji fedha *(cash flow plan*) uliowekwa;

ii. Kiasi cha Fedha kinachotolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ni kikubwa ikilinganishwa na matumizi ya maendeleo; na

iii. Fedha hazipatikani kwa wakati, jambo linaloathiri utekelezaji wa mipango ya bajeti kwa Ofisi hii.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, hadi kufikia mwezi Februari, 2018 Ofisi ya Rais – TAMISEMI pamoja na Taasisi zilizo chini yake, ilikuwa imepokea **Shilingi 245,177,039,868.65/=** kutoka Hazina kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kiasi hicho ni sawa na **asilimia 53** ya fedha yote iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Ofisi hii.

Mwenendo wa upatikanaji wa fedha unaonesha kwamba, kiasi hicho kilichopatikana katika kipindi hicho kimepungua kwa takribani asilimia 4 ikilinganishwa na kipindi kama hicho katika Mwaka wa Fedha wa 2016/2017 ambapo ilikuwa ni asilimia 57.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa fedha za matumizi ya kawaida hadi kufikia februari, 2018 kiasi kilichokuwa kimepokelewa ni **Shilingi 29,072,505,060.65,** sawa na asilimia 69 ya fedha iliyoidhinishwa. Kwa kulinganisha na kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha uliopita wa 2016/17 kiasi hicho kimeongezeka kwa asilimia 5 kutoka asilimia 64.

Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo uchambuzi umebaini kwamba, hadi kufikia mwezi Februari, 2018, Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Taasisi zake ilikuwa imepokea jumla ya **shilingi 216,104,534,808.00** kutoka Hazina, sawa na asilimia 52 ya fedha yote iliyoidhinishwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo katika kipindi hicho. Kiasi hicho kimepungua kwa takribani asilimia 4 ikilinganishwa na kiasi kilichopokelewa katika kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2016/17 ambacho kilifikia asilimia 56 ya lengo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba kwa wastani wa upatikanaji wa fedha (Matumizi ya Kawaida na Maendeleo) katika Mwaka wa Fedha 2017/18 ulikuwa ni **asilimia 60.5**, kiwango ambacho ni sawa na kilichoshuhudiwa katika Mwaka wa Fedha 2016/17.

Kwa tafsiri ya kawaida ni kwamba, bado upatikanaji wa fedha umeshindwa kufikia lengo la angalau asilimia 25 kwa kila robo ya mwaka wa fedha, ambapo ingepaswa kuwa zaidi ya asilimia 70.

Aidha, bado upatikanaji wa fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida umeendelea kuwa juu ikilinganishwa na fedha zinazotolewa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Hii inaashiria kwamba miradi ya maendeleo itaendelea kuathirika kutokana na kuchelewa kwa fedha. Na hali hiyo, inaweza kuwaingiza Watendaji wa Halmashauri katika migogoro na Watoa huduma na Wakandarasi kutokana na kushindwa kulipwa kwa wakati, baada ya kuwa wamekamilisha kazi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya ulinganisho wa uwiano wa fedha iliyoidhishwa kwa ajili ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI na fedha iliyopatikana hadi kufikia mwezi Februari, 2018, kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Ufafanuzi zaidi wa ulinganisho huu umeoneshwa kupitia **Jedwali Na. 01**

**Jedwali Na.01:** Bajeti iliyoidhinishwa ikilinganishwa na Fedha zilizopatikana hadi Februari, 2018

| Mgawanyo wa Bajeti | Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/18 | Kiasi kilichopokelewa hadi Februari, 2018 | Asilimia ya Kiasi kilichopokelewa hadi Februari,2018 |
|---|---|---|---|
| OC | 23,810,002,200.00 | 14,944,710,887.80 | 63 |
| Mishahara | 18,347,579,957.00 | 14,127,794,172.85 | 69 |
| Maendeleo | 417,256,688,000.00 | 216,104,534,808.00 | 52 |
| **Jumla** | **459,414,270,157.00** | **245,177,039,868.65** | **53** |

**Chanzo:** Randama ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI (2017/2018)

3.1.3 **Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, katika mapitio na uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Kamati ilitoa maoni na ushauri wa mambo kumi na mbili (12) ili yaweze kuzingatiwa katika utekelezaji vipaumbele vya bajeti ya Ofisi hii kuleta ufanisi na maendeleo;

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Kamati baada ya kupitia majibu yaliyowasilishwa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeridhishwa na jitihada za Serikali katika kuzingatia ushauri na maoni ya Kamati kwa kutatua changamoto zilizobainishwa.

Kuzingatiwa kwa maoni na ushauri wa Kamati kumechangia uboreshaji wa huduma za msingi kwa maendeleo ya Jamii. Hata hivyo, bado Kamati inaitaka Serikali kuendelea kufanyia kazi ushauri kwa baadhi ya maeneo ili kuendelea kuboresha utoaji wa huduma kwa Wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** baadhi ya maeneo ambayo yameboreshwa kwa kuzingatia ushauri na maoni ya Kamati ni pamoja na:-

i. Halmashauri kubuni vyanzo vipya vya mapato ili kuepuka utegemezi wa ruzuku kutoka Serikali Kuu, ambapo Ofisi ya Rais TAMISEMI imezielekeza Halmashauri kubuni miradi ya kimkakati kwa lengo la kuongeza mapato ya ndani. Hadi kufikia Februari, 2018 Halmashauri 21 ziliweza kubuni miradi mbalimbali kama vile ujenzi wa stendi za mabasi, masoko, maeneo ya maegesho, machinjio na kilimo cha umwagiliaji ambayo imekidhi vigezo vya kupata fedha kwa ajili ya utekelezaji. Aidha, Serikali imetenga kiasi cha Shilingi **Bilioni 131.5** katika mwaka ujao wa fedha kwa ajili ya Halmashauri hizo;

ii. Serikali ihakikishe Halmashauri zote zinatumia Mfumo wa kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato ya ndani *(Local Governemnt Revenue Collection Information System - LGRCIS)*, ambapo hadi kufikia Disemba, 2017 Halmashauri zote 185 sawa na asilimia 100 zilikuwa zimeanza kutumia

Mfumo huu katika ukusanyaji wa mapato. Aidha, karibu kila Halmashauri imetenga fedha kwa ajili ya ununuzi wa mashine za kukusanyia mapato (POS) kwa lengo la kuimarisha mfumo huo.

**Mheshimiwa Spika,** yapo baadhi ya maoni ambayo licha ya kufanyiwa kazi na Serikali, bado Kamati inaona kuna umuhimu wa kuendelea kuyaboresha zaidi ili kuleta ufanisi katika utendaji. Maoni hayo ni pamoja na:-

i. Kuhakikisha Halmashauri zinaandaa na kutunza takwimu sahihi kuhusiana na namba vikundi vya Wanawake na Vijana, vinavyopokea na kurejesha fedha zinazotokana na Asilimia kumi (10%) ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri;

   Aidha, Halmashauri zitekeleze kwa ukamilifu utengaji wa fedha hizo na kuzipeleka kwa wahusika. Taarifa zinaonesha kwamba, hadi kufikia mwezi Februari, 2018 utengaji wa fedha hizo ulikuwa ni asilimia 25.5, kiwango ambacho kiko chini sana. Ni ushauri wa Kamati kwamba, jambo hili linahitaji msisitizo wa Serikali;

ii. Halmashauri kushirikiana na Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) kuandaa mpango wa matumizi bora ya Ardhi, kwa kuainisha maeneo ya Kilimo, Ufugaji na matumizi mengine, jambo litakalosaidia kuepusha migogoro ya ardhi baina ya Wakulima na Wafugaji; na

iii. Serikali kutoa fedha za Miradi ya Maendeleo kwa wakati ili kuwezesha Halmashauri kulipa madeni ya Watoa huduma na Wakandarasi kwa wakati na hivyo

kuepusha ongezeko la gharama katika miradi inayotekelezwa. Kiasi cha fedha kilichopokelewa na Halmashauri kwa ajili ya maendeleo (asilimia 51) kinaashiria kwamba, utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Halmashauri utaendelea kuathirika.

## 4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

### 4.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Mpango wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2018/2019, kwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, inayojumuisha Mafungu 28 (Fungu 56; Fungu 02 na Mafungu 26 ya Mikoa) imeandaliwa kwa kuzingatia yafuatayo :-

i. Mwongozo wa Taifa wa kuandaa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na maelekezo mbalimbali ya Viongozi wa Kitaifa;

ii. Vipaumbele vilivyoanishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2015 – 2020; na

iii. Malengo Endelevu ya Maendeleo *(Sustainable Development Goals*); na Mpango Mkakati wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI uliofanyiwa mapitio mwaka 2016.

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha unaokuja 2018/2019, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuimarisha amani na utulivu nchini, kusimamia shughuli za utawala bora, kukuza demokrasia, ushirikishwaji wa Wananchi na Ugatuaji wa Madaraka kwa Umma (D by D);

ii. Kusimamia matumizi ya rasilimali katika ngazi zote za Ofisi ya Rais – TAMISEMI;

iii. Kusimamia utekelezaji wa majukumu ya msingi (Core Business) ya kila Taasisi yaliyoainishwa kwenye Mipango Mikakati yao;

iv. Kuchochea na kuhimiza ukuaji wa Uchumi kwa maendeleo ya Wananchi na Taifa kwa ujumla kwa kuiwezesha Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuweka mazingira mazuri ya Biashara na Uwekezaji hasa katika Kilimo na Viwanda;

v. Kusimamia utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI ikiwa ni pamoja na kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa shughuli za Serikali, programu na miradi katika ngazi ya Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

vi. Kuratibu shughuli za usimamizi na uendeshaji wa elimu, afya, maji, kilimo, mifugo, uvuvi na sekta nyingine;

vii. Kuratibu shughuli za kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa Watumishi wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na kuendeleza Rasilimali Watu kwa kuwaongezea ujuzi na vitendea kazi;

viii. Kusimamia, kuratibu na kuwezesha utekelezaji wa Taasisi, programu na miradi iliyo chini ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI; na

ix. Kusimamia maandalizi ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika mwaka 2019.

**Mheshimiwa Spika,** ili kutekeleza malengo hayo yaliyokusudiwa, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mikoa na Halmashauri, zinaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 6,582,946, 851,733/=**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 4,522,965,704,000/=** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, na **Shilingi 1,799,436,057,500/=** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Aidha, katika fedha za matumizi ya kawaida, **Shilingi 4,134,200,811,930/=** sawa na asilimia 62.8 ni kwa ajili ya Mishahara, na **Shilingi 649,309,982,303/=** sawa na asilimia 9.8 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. **Jedwali Na. 02** linafafanua zaidi juu ya Bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

**Jedwali Na. 02** Mgawanyo wa Bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa Mwaka wa Fedha 2018/19

| Mgawanyo wa Bajeti | Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/19 | Asilimia ya Makadirio (%) |
|---|---|---|
| OC | 649,309,982,303 | 9.8 |
| Mishahara | 4,134,200,811,930 | 62.8 |
| Maendeleo | 1, 799, 436, 057,500 | 27.3 |
| **Jumla** | 6, 582,946, 851,733 | **100** |

**Chanzo:** Randama ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI (2018/2019)

## 4.2 Uchambuzi wa makadirio ya Mapato

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, inakadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 758,362,711,799.** Mapato hayo yameongezeka kwa **Shilingi 44,778,191,187** sawa na **asilimia 5.9** ikilinganishwa na makusanyo ya Mwaka wa Fedha 2017/2018 kwa mgawanyo utakaooneshwa katika **Jedwali Na. 03** hapo chini.

**Mheshimiwa Spika,** makusanyo hayo yanatarajiwa kutokana na kuuza vifaa chakavu pamoja na nyaraka za zabuni, faini mbalimbali, marejesho ya masurufu na mishahara. Aidha, kwa upande wa Halmashauri, makusanyo yatatokana na ushuru na kodi mbalimbali na vyanzo vingine vya mapato vilivyopo kwa mujibu wa sheria.

**Jedwali Na.3 Mchanganuo wa Maduhuli na Makusanyo ya ndani**

| Ofisi/ Taasisi | Bajeti 2017/18 | Bajeti 2018/19 | Tofauti | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| OR – TAMISEMI na Taasisi | 22,766,063,908 | 22,643,519,091.00 | 122,544,817 | 0.53 |
| Mikoa | 3,511,759,704 | 130,563,708.00 | 3,381,195,996 | 96.2 |
| Halmashauri | 687,306,661,000 | 735,588,629,000.00 | 48,281,968,000 | 6.5 |
| **Jumla** | 713,584,520,612 | 758,362,711,799.00 | 44,778,191,187 | **5.9** |

**Chanzo:** Randama ya Ofisi ya Rais –TAMISEMI (2018/2019)

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa uchambuzi huu makusanyo yote yameongezeka kwa **Shilingi 44,778,191,187** ikilinganishwa na mwaka wa fedha unaomalizika. Kiasi hicho ni sawa na ongezeko la asilimia 5.9. Aidha, ongezeko hilo linarajiwa kuchangiwa kwa kiasi kikubwa na Halmashauri nchini ambazo maduhuli yanayotarajiwa kukusanywa yameongezeka kwa takribani **Shilingi 48,281,968,000** sawa na asilimia 6.5 ikilinganishwa na makusanyo ya Halmashauri katika Mwaka wa Fedha unaoisha.

Ni mtazamo wa Kamati kwamba, huenda sababu ya ongezeko hilo ni kwamba, Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeendelea kuimarisha matumizi ya mashine za kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato. Aidha, ni wazi kwamba watu wengi na vyanzo vingi vya mapato vinapatikana katika mamlaka za Serikali za Mitaa.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kubainika kwa ongezeko la jumla la **asilimia 5.9** ikilinganishwa na makusanyo ya mwaka unaomalizika, makusanyo ya Mikoa yamebainika kushuka kwa kiwango cha kutisha cha asilimia 96.2 (Shilingi 3,381,195,996).

Kamati ilipotaka maelezo ya kwanini mapato ya Mikoa yameshuka kwa kiwango hicho, ilielezwa kwamba sababu ni Hospitali za Rufaa za Mikoa kuhamishiwa Wizara ya Afya na hivyo makusanyo yote yaliyokuwa yakikusanywa kwa mfumo wa GoT – HoMIS kuondoka.

## 4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Ofisi ya Rais -TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa, kwa pamoja zinaomba kuidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya **Shilingi 6, 582,946, 851,733** kwa ajili ya kutekeleza majukumu mbalimbali ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kati ya fedha hizo **Shilingi 4,522,965,704,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 1,799,436,057,500** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Aidha, katika fedha hizo zinazoombwa kuidhinishwa, **Shilingi 12, 515,260,520** ni kwa ajili ya Mishahara na Matumizi Mengineyo kwa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC).

**Mheshimiwa Spika**, kiasi cha Fedha kinachoombwa kuidhinishwa kimeongezeka kwa **Shilingi 4,319,381,367** sawa na asilimia 0.07 ikilinganishwa na bajeti ya Mwaka wa Fedha 2017/2018. Hata hivyo, ongezeko la Mwaka huu ni dogo sana ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2017/18 ambapo ongezeko lilikuwa asilimia 8.52%.

Uchambuzi umebaini kwamba, katika fedha za Miradi ya Maendeleo, kuna ongezeko la asilimia 0.91 kutoka **Shilingi 1,783,206,586,000** katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 hadi **Shilingi 1,799,436,057,500** katika Mwaka wa fedha 2018/2019.

Uchambuzi umebaini kwamba, ongezeko la bajeti yote pamoja na ile ya maendeleo katika kipindi cha miaka mitatu limekuwa ni likiongezeka kwa kupungua (increasing at decreasing rate). i.e. kutoka asilimia 12 mwaka 2016/17, asilimia 8.5 mwaka 2017/18 na asilimia 0.07 kwa mwaka wa fedha 2018/19.

**Mheshimiwa Spika,** katika kulinganisha bajeti ya Ofisi ya Rais TAMISEMI na Bajeti ya Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2018/19 uchambuzi ulibaini kwamba, wakati bajeti ya Taifa ikiongezeka kwa asilimia 2.53 kwa Mwaka wa Fedha 2018/19 ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2016/17, bajeti ya TAMISEMI katika kipindi hicho imeongezeka kwa asilimia 0.07.

Aidha, uchambuzi umebaini zaidi kwamba, bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI ni sawa na **asilimia 20.27** ya bajeti ya Taifa. Uwiano huo umeendelea kupungua katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, kutoka Mwaka wa Fedha 2015/16 ambapo uwiano ulikuwa **asilimia 24** hadi kiwango hicho cha sasa.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kupungua huko, bado ni jambo lisilopingika kwamba, Ofisi ya Rais TAMISEMI ndiyo Wizara inayobeba sehemu kubwa ya bajeti ya nchi yetu ikilinganishwa na Wizara nyingine, kutokana na kusimamia kila Sekta katika ngazi za Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Ni kwa mantiki hiyo, Kamati ingetamani kuona Ofisi hii inaongezewa fedha katika bajeti yake.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, mgawanyo wa makadirio ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa ni kama unavyooneshwa katika **Jedwali Na.4** ambalo ni Kiambatisho "**A"** cha Taarifa hii.

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kufanya ziara kwenye miradi ya Maendeleo na kupitia Taarifa ya utekelezaji wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na Taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, Kamati inatoa maoni na ushauri kama ifuatavyo:-

i. Serikali ihimize Halmashauri kubuni vyanzo vipya vya mapato ili kufidia pengo kubwa la mapato lililotokana na Serikali Kuu kuchukua baadhi ya vyanzo vilivyokuwa tegemezi kwa Halmashuri nchini kama vile kodi ya majengo *(property tax)*. Kamati imebani kushuka kwa kiwango cha kutisha kwa makusanyo ya ndani ya kwa baadhi ya Halmashauri ambapo hadi mwezi Februari, 2018 (ikiwa ni robo ya tatu) Halmashauri hizo zilishindwa kufikia asilimia 25 ya makusanyo. Mingoni mwa Halmashauri hizo ni Mbinga DC (13%), Siha DC (20%) na Mji Kishapu (23%).

ii. Serikali itenge fedha za kutosha ili kukamilisha ujenzi wa maboma, katika Halmashauri nchini ambayo yamejengwa kwa kushirikisha nguvu za Wananchi. Kuendelea kuyaacha majengo hayo bila kuyakamilisha kunawakatisha tamaa Wananchi kushiriki katika kazi za maendeleo, na kuwafanya waendelee kukosa huduma muhimu za kijamii ambazo wanazitegemea.

iii. Serikali iangalie uwezekano wa kupunguza au kuondoa kodi ya taulo za kike *(tampon tax)* ili kuwawezesha Watoto wa Kike hasa kutoka familia maskini kumudu gharama ya taulo hizo na kuweza kuhudhuria masomo kikamilifu.

Aidha, Serikali iweke mkakati wa kuanzisha viwanda vya ndani kwa ajili ya kuzalisha taulo hizo *(tampons)* kutokana na fursa ya malighafi ya pamba inayozalishwa kwa wingi nchini.

Utafiti wa Shirika la Umoja Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) mwaka 2008 ulibaini asilimia 10 ya watoto wa kike wanaodahiliwa katika elimu ya msingi na sekondari katika nchi za kusini mwa Jangwa la Sahara *(Sub Saharan Countries)* huacha masomo kwa sababu ya kukosa au kushindwa kumudu gharama za taulo za kike *(pads/tampons).*

Aidha, utafiti wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) ulibaini kwamba, kutokana na kushindwa kumudu gharama za taulo za kike, Wanafunzi wa kike wamekuwa wakikumbwa na athari za kushindwa kuhudhuria masomo kwa siku kati ya 3 hadi 5 kwa mwezi, kupata mimba za utotoni na ufaulu hafifu.

Baadhi ya nchi barani Afrika, kama vile Kenya, Mauritius na Shelisheli zimefanikiwa kupunguza kwa kiwango kikubwa kadhia hiyo kwa watoto wa kike;

iv. Serikali iendeleze ujenzi wa wodi maalum (mama ngojea) ili kuwezesha Wajawazito wanaotoka mbali na maeneo ya huduma za afya, kupata uangalizi wa karibu kutoka kwa Wataalam wa afya wanapokaribia kujifungua. Hatua hiyo itasaidia kupunguza vifo vya Mama na Mtoto wakati wa kujifungua *(maternity motarity deaths)*

ambavyo huchangiwa na kukosa huduma za msingi za afya kama vile upasuaji *(operation)*.

v. Serikali ihimize Halmashauri nchini kuchangia kikamilifu katika Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa, kwani nyingi zimeshindwa kufanya hivyo. Hadi kufikia Februari, 2018 Halmashauri zilikuwa zimechangia **Shilingi Bilioni 1.11** tu sawa na asilimia 20 ya makadirio ya kiasi kilichopaswa kuchangiwa. Hali hiyo inakwamisha bodi hiyo kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

vi. Serikali isaidie Mikoa na Halmashauri mpya nchini kupata majengo ya Ofisi, Watumishi na vitendea kazi na kuboreshewa miundomibu ya barabara ili lengo la kuanzishwa kwake liweze kufikiwa. Ni wazi kuwa maeneo hayo mapya ya utawala yalianzishwa kwa lengo la kusogeza huduma za kijamii karibu na Wananchi na kuhamasisha maendeleo katika maeneo husika. Mfano wa maeneo hayo ni Mikoa ya mipya ya Katavi, Njombe na Songwe;

vii. Ofisi ya Rais, TAMISEMI iendelee kutoa ufafanunuzi wa Agizo la Mheshimiwa Rais kuhusu michango ya Wazazi katika Shule za Serikali za Msingi na Sekondari nchini. Bado jambo hili linaendelea kuleta mkanganyiko miongoni mwa Wazazi na Walimu, na linaathiri utoaji wa elimu katika baadhi ya maeneo ambayo Wazazi walikuwa wameamua wenyewe kuchangia elimu.

viii. Ofisi ya Rais, TAMISEMI isimamie na kuhakikisha Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri nchini zinazingatia kikamilifu Waraka unaozitaka kuzingatia ushiriki wa Wabunge katika vikao vya kazi

na ushauri vya Mkoa, Wilaya na Halmashauri *(RCC, DCC, Full Council and Finance Committee)*. Waraka huo unazitaka Sekretarieti hizo kupanga ratiba za vikao hivyo bila kuingiliana na Vikao vya Bunge. Aidha, hatua kali zichukuliwe dhidi ya watakaoendelea kukiuka masharti ya waraka huo;

ix. Serikali ichukue hatua za makusudi ili kukabili tatizo la ucheleweshaji na upatikanji wa fedha kutoka Hazina *(disbursement)*, kwani unaathiri mtiririko wa bajeti *(cash flow plan)* na hivyo kukwamisha utekelezaji wa malengo na mipango mingi ya Serikali. Aidha, Serikali iweke vipaumbele vichache ambavyo itamudu kuvitekeleza kwa kuzingatia uwezo wa kibajeti uliopo;

x. Serikali iendelee kuzisisitiza Halmashauri kutenga asilimia kumi (10%) ya makusanyo yake ya ndani kwa ajili ya kuwezesha kiuchumi Wanawake na Vijana. Aidha, hatua kali zichukuliwe kwa Halmashauri ambazo zimeendelea kupuuza agizo hilo.

xi. Serikali iandae na kuwasilisha Bungeni Muswada wa kusudio la kutunga Sheria itakayowezesha kusimamia kikamilifu utengaji, utoaji na urejeshaji wa fedha zinazotokana na asilimia kumi (10%) ya mapato ya ndani ya Halmashauri kwa ajili ya kuwezesha kiuchumi Wanawake na Vijana;

xii. Serikali isimamie kikamilifu Halmashauri ili kuhakikisha zinaboresha mazingira ya kutolea elimu kwa kujenga miundombinu ya kielimu hasa vyumba vya madarasa na matundu ya vyoo, ambayo upungufu wake unachangia kuathiri utoaji wa elimu. Ni aibu katika karne hii Walimu na Wanafunzi kuchangia matundu ya vyoo. Aidha, uchache wa matundu ya vyoo unachangia watoto kuacha masomo *(drop outs)* kutokana na kushindwa kujisitiri wanapokuwa katika siku zao;

xiii. Kamati inapongeza hatua ya Serikali kuanzisha Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) kwani utasaidia sana kuboresha na kuendeleza miundombinu ya barabara katika Miji na Vijiji. Hata hivyo, bado kuna changamoto ya fedha kidogo inayopelekwa kwa Wakala hii. Kamati inashauri mgawo wa fedha za Mfuko wa Barabara (road fund) kwa ajili ya TARURA uongezeke kutoka asilimia 30 ya sasa hadi 50.

xiv. Serikali iiwezeshe TARURA kuajiri Watumishi wa kutosha hasa wa kada za uhandisi ili kuondoa changamoto ya Wakala kuchukua Watumishi wa Halmashauri na hivyo kuathiri utendaji wa Halmashauri hizo.

xv. Ofisi ya Rais – TAMISEMI ihakikishe TARURA inashirikisha Halmashauri (Watendaji, Madiwani na Wabunge) katika shughuli inazopanga kutekeleza ili kuondoa mkinzano ambao umeshuhudiwa kwa baadhi ya Halmashauri nchini kutoelewa shughuli zinazopangwa kutekelezwa na Wakala huo katika maeneo yao.

## 6.0 **HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwako binafsi, Naibu Spika, na Wenyeviti wa Bunge, kwa namna mnavyoendesha shughuli za Bunge. Aidha, nawapongeza Wenyeviti wa Bunge wote kwa kuchaguliwa tena kuendelea na nafasi zao. Hii ni ishara kwamba, utendaji wao katika kipindi kilichopita ulikuwa mzuri na ndiyo umewapa imani Waheshimiwa Wabunge kuweza kuwachagua tena.

Aidha, nawashukuru kwa dhati Wajumbe wote wa Kamati kwa kutuchagua tena mimi na Makamu Mwenyekiti, Mhe. Mwanne Ismail Mchemba (Mb) ili tuendelee kuongoza Kamati kwa kipindi kilichosalia cha uhai wa Bunge. Hii ni ishara kwamba, wanatuamini na wako tayari kushirikiana nasi katika kutekeleza shughuli za Kamati. Ninatambua kwamba, "cheo sio fursa bali ni dhamana" na "ukiaminiwa basi nawe unapaswa kujiamini." Tunalo deni kwa Wajumbe, na njia pekee ya kulipa deni hilo ni kuenzi imani na ushirikiano wao kwetu, kwa kuwatumikia kikamilifu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati hii ina Mafungu mengi ya Bajeti ambayo inayashughulikia, na kwa kuzingatia muda mfupi uliokuwa umetengwa wakati wa uchambuzi wa bajeti, Wajumbe walilazimika kufanya kazi kwa saa nyingi wakati mwingine hadi jioni. Hata hivyo, mazingira hayo hayakuwa kikwazo kwa Wajumbe, kwani walitekeleza wajibu wao kwa moyo na weledi wa hali ya juu. Hii ni ishara ya utayari wao katika kuwatumikia Wananchi, Bunge na Taifa kwa ujumla.

Kwa umuhimu wa namna ya pekee ningetamani sana kuwatambua kwa kuwataja majina yao. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa muda naomba

majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard). Majina hayo ni haya yafuatayo:-

1. Mhe. Jasson Samson Rweikiza, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe.Mwanne Ismail Mchemba,Mb – Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Margaret Simwanza Sitta, Mb,
4. Mhe. Angelina Adam Malembeka Mb
5. Mhe.George Malima Lubeleje,Mb
6. Mhe. Hamad Salim Maalim,Mb
7. Mhe.Waitara Mwita Mwikwabe,Mb
8. Mhe. Innocent Sebba Bilakwate,Mb
9. Mhe. Mwatum Dau Haji,Mb
10. Mhe. Saada Mkuya Salum,Mb
11. Mhe. Salum Khamis Salum,Mb
12. Mhe. Venance Methusela Mwamoto,Mb
13. Mhe. Mussa Ramadhani Sima, Mb
14. Mhe. Anna Joram Mhagama, Mb
15. Mhe. Jerome Dismas Bwanausi, Mb
16. Mhe. Martha Moses Mlata, Mb
17. Mhe. Lusia Ursula Michael, Mb
18. Mhe. Rehema Juma Migilla, Mb
19. Mhe. Joseph Raman Selasini, Mb
20. Mhe. Joel Mwaka Makanyaga, Mb
21. Mhe. Philipo Augustino Mulugo, Mb
22. Mhe. Khatib Said Haji, Mb
23. Mhe. Njalu Daudi Silanga, Mb
24. Mhe. Daniel Edward Mtuka, Mb
25. Mhe. Hamidu Hassan Bobali, Mb

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Kamati napenda kumshukuru sana Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mhe. Seleman Said Jafo (Mb) kwa ushirikiano mkubwa aliouonesha kwa Kamati hii ambao umechangia kwa sehemu kubwa kwa Kamati kutekeleza shughuli zake. Yeye pamoja na Naibu Mawaziri wake, Mhe. George Joseph Kakunda (Mb) na Mhe. Josephat Sinkamba Kandege (Mb) ni hazina kubwa katika ustawi wa Serikali za Mitaa na maendeleo ya Taifa hili.

Nawashukuru pia watendaji wote wa Ofisi hii wakiongozwa na Mhandisi Musa Iyombe, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa ushirikiano wao kwa Kamati wakati wote wa kuchambua Taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi Rais, TAMISEMI kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Aidha, nawashukuru Wakuu wa Mikoa yote ya Tanzania Bara, Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri zote nchini, kwa utendaji wao uliotukuka katika utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa fedha unaoisha, na kwa uwasilishaji mzuri wa Taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka ujao wa fedha.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee namshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Stephen Kagaigai, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Husein, Mkurugenzi Msaidizi, Ndg. Angelina Sanga, Makatibu wa Kamati hii Ndg. Chacha Nyakega, Ndg. Victor Leonard na Ndg. Eunike Shirima, wakisaidiwa na Ndg. Catherine Kitutu, kwa uratibu mzuri wa shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya Taarifa hii. Vilevile, nawashukuru Watumishi

wote wa Idara ya Taarifa Rasmi za Bunge, wakiongozwa na Bi. Hanifa Masaninga, kwa kuandaa na kutoa Vitabu vya taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja hapo awali.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Jasson S.Rweikiza (Mb)
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA**
**NA SERIKALI ZA MITAA**

11 Aprili, 2018

**KIAMBATISHO "A"**

**Jedwali Na 4:** Mgawanyo wa makadirio ya Bajeti ya OR- TAMISEMI, Mikoa na Halmashauri kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 ikilinganishwa na Mwaka 2017/18

| Eneo la Matumizi | Makadirio 2017/2018 | Makadirio 2018/2019 | Tofauti | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| **Matumizi ya Kawaida** | | | | |
| **Mishahara:** | | | | |
| OR – TAMISEMI (HQ) | 8,491,975,000 | 8,736,397,905 | 244,422,905 | 2.79 |
| Taasisi | 15,318,027,000 | 14,916,444,000 | 401,583,000 | 2.62 |
| Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) | 7,800,146,000 | 7,893,115,025 | 92,969,025 | 1.17 |
| Mikoa | 168,579,832,000 | 159,941,766,000 | 8,638,066,000 | 5.12 |
| Halmashauri | 4,075,783,400,000 | 3,942,713,089,000 | 133,070,311,000 | 3.62 |
| **Jumla ndogo Mishahara** | **4,275,973,380,200** | **4,134,200,811,930** | **141,772,568,270** | **3.31** |
| | | | | |
| **Matumizi Mengineyo:** | | | | |
| OR – TAMISEMI (HQ) | 6,384,731,523 | 17,896,530,002 | 11,511,798,479 | 180.32 |
| Taasisi | 1,827,564,148 | 1,318,870,806 | 508,693,342 | 27.83 |
| Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) | 4,622,145,495 | 4,622,145,495 | 0 | 0 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Mikoa | 41,297,783,000 | 45,219,821,000 | 3,922,038,000 | 9.49 |
| Halmashauri | 465,315,280,000 | 580,252,615,000 | 114,937,335,000 | 24.73 |
| **Jumla Matumizi Mengineyo** | **519,447,504,166** | **649,309,982,303** | **129,862,478,137** | **25** |
| **Jumla Matumizi ya Kawaida** | **4,795,420,884,366** | **4,783,510,794,233** | **11,910,090,133** | **0.24** |
| | | | | |
| **Fedha za Maendeleo:** | | | | |
| OR – TAMISEMI | 417,256,688,000 | 345,113,541,000 | 72,143,147,000 | 17.28 |
| Mikoa | 75,259,322,000 | 93,184,414,000 | 17,925,092,000 | 23.81 |
| Halmashauri | 1,290,690,576,000 | 1,361,138,102,500 | 70,447,526,500 | 5.46 |
| **Jumla ya Maendeleo** | **1,783,206,586,000** | **1,799,436,057,500** | **16,229,471,500** | **0.91** |
| **JUMLA KUU** | **6,578,627,470,366** | **6,582,946,851,733** | **4,319,381,367** | **0.07** |

**Chanzo:** Randama ya TAMISEMI (2018/2019)